

Ufundishaji wa Kiswahili na Changamoto zake Mintarafu Chuo Kikuu cha Moi

Makoti Vifu

Chuo Kikuu cha Machakos

Ikisiri

Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu ulisisitizwa sana na Tume ya MacKay (1981) iliyopelekea kuanzishwa Chuo Kikuu cha Pili nchini Kenya. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret ndicho Chuo Kikuu cha pili kuanzishwa baada ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Chuo Kikuu cha Moi kilianzisha mafunzo ya Kiswahili mwaka wa 1987 kwa wanafunzi wa shahada ya ualimu hadi leo, wakiwemo wanafunzi wa shahada ya Kiswahili chini ya Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika. Idara hii leo imetimia miaka thelathini (30) tangu kuzinduliwa kwake. Kwa hiyo, kimantiki, inatarajiwa iwe imeimarika katika vitabu vya kufundishia na marejeleo, na kuwa na walimu wa kutosha. Maswali ya kudadisi ni: Je, haya yametimia? Je, wanafunzi wanaojungu na idara hii na kupata mafunzo ya Kiswahili wana umilisi wa kimsingi kukabiliana na mtalaa wa somo hili katika kiwango cha shahada? Makala haya yanapigia mbizi maswali haya na kuweka bayana changamoto zinazomkumba mwalimu wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Maneno Muhimu: *Ufundishaji wa Kiswahili, Changamoto, Chuo Kikuu cha Moi*

Utangulizi

Makala haya yanachunguza na kujadili matatizo mbalimbali yanayomkumba mwalimu wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. Kiswahili ni somo ambalo linafundishwa kutoka shule za msingi hadi chuo kikuu katika viwango vya: shahada, uzamili na uzamifu. Makala haya yanadadisi ufundishaji wa shahada kwa wanafunzi waliopo kwa sasa hivi. Mtafiti alichunguza kazi za wanafunzi wa miaka yote minne kama data yake na kutalii maktaba ya Margret Thatcher ya Chuo Kikuu cha Moi. Alifanya hivi ili kubaini mchango wa maktaba hii katika ufundishaji wa Kiswahili.

Vifupisho vifuatavyo vimetumika katika makala haya:

E.A.C.E East Africa Certificate of Education (mtihani wa mwisho wa kidato cha nne).

C.P.E Certificate of Primary Education (mtihani wa mwisho wa darasa la saba).

8-4-4 Miaka minane shule ya msingi, minne shule ya upili, minne chuo kikuu.

K.C.P.E Kenya Certificate of Primary Education (mtihani wa mwisho wa darasa la nane).

K.C.S.E Kenya Certificate of Secondary Education (mtihani wa mwisho wa kidato cha nne).

KN Kundi/Kirai Nomino.

Kiswahili na Ufundishaji wake

Kiswahili ni lugha inayotumika kama *lingua franca* Afrika Mashariki na kati. Ina wazungumzaji takribani milioni saba (Chimera, 1998). Nchini Kenya, Kiswahili kilianza kufundishwa tangu enzi za ukoloni katika shule za msingi lakini hakikutahiniwa. Kenya ilipopata uhuru (1963), ufundishaji wa Kiswahili uliendelea. Serikali ya Kenya ikaunda Tume ya Ominde (1964) kuchunguza mfumo wa elimu nchini Kenya na ilipitisha Kiswahili kiendelee kufundishwa mionganoni mwa maazimio mengine lakini kisitahiniwe mwisho wa mtalaa (Ogechi, 2004). Katika shule za upili, kiliendelea kufundishwa kama somo lisilo la lazima na kutahiniwa mwisho wa kidato cha nne (E.A.C.E). Mwaka wa 1976, Tume ya Gachathi iliundwa kuchunguza mfumo wa elimu nchini Kenya na ilipitisha Kiswahili kifundishwe katika shule za msingi na kitahiniwe katika mtihani wa mwisho wa darasa la saba (C.P.E) (Eshiwani 1993; Ogechi 2004). Hata hivyo, hili halikufanyika hadi agizo la Rais Mstaafu, Daniel Arap Moi, 1983, na kujiri kwa mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4 (Mackay, 1981; Eshiwani, 1993; Chimera, 2000).

Kwa sasa, nchini Kenya, Kiswahili kinafundishwa takriban katika Vyuo Vikuu vyote na Vyuo Andamizi: Vyuo Vikuu vya Nairobi, Moi, Kenyatta, Maseno, Masinde Muliro mionganoni mwa vingine vingi. Chimera (2000) anaeleza kuwa Kiswahili kinafundishwa katika Vyuo Vikuu mbalimbali ulimwenguni. Anasema Kiswahili kinafundishwa katika takriban Vyuo Vikuu 100 nchini Marekani, vikiwemo vile vya kifahari kama Havard, Yale, Cornell, U.C.L.A na vinginevyo. Vyuo vingine ni Vyuo Vikuu vya London, York na Cambridge huko Uingereza. Pia kuna Vyuo Vikuu nchini Ujeruman, Korea Kusini, Libya, Ghana na Japan vinavyofundisha Kiswahili kama lugha ya Kigeni. Hii inadhihirisha kuwa Kiswahili ni somo na lugha muhimu inayotambuliwa ulimwenguni kote. Hivyo wasomi na wanafunzi wa Kiswahili Afrika ya Mashariki hawana budi kukifahamu Kiswahili barabara na kuwa na umilisi wa kuridhisha.

Mfumo wa elimu wa 8-4-4 ultia nguvu somo la Kiswahili katika historia ya elimu nchini Kenya. Mfumo huu ulifanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za msingi na upili nchini na kutahiniwa katika mtihani wa darasa la nane (K.C.P.E) na ule wa kidato cha nne (K.C.S.E). Odeo (2002) anatueleza umuhimu uliopewa Kiswahili katika mtalaa wa elimu: Kama somo Kiswahili kinapata msisitizo mwingu katika mtalaa wa shule nchini Kenya ambapo kwa sasa hivi kimepewa vipindi sita kwa wiki katika vidato vya tatu na nne katika shule za sekondari.

Kwa hiyo, mwanafunzi kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu, huwa amesoma Kiswahili kwa miaka kumi na miwili (12). Muda huu si mfupi; unatosha kwa mwanafunzi kuwa na umilisi wa kimsingi katika lugha hii. Mwanafunzi anatarajiwa kuvimilisi vipengele mbalimbali kama vile uambilishi, umilikishi, urejeshi, uonyeshi, umoja na wingi, njeo katika Kiswahili. Huu ndio msingi wa lugha yoyote ile. Aidha, lazima mwanafunzi awe na umilisi wa fonolojia ya Kiswahili. Fonolojia itamsaidia mwanafunzi kutamka msamati wa Kiswahili kwa usahihi.

Katiba ya Kenya (2010) iliinua hadhi ya Kiswahili kwa kuifanya lugha rasmi pamoja na Kiingereza. Kwa hiyo, ni wajibu wa wakereketwa na wasomi wa Kiswahili huhakikisha kuwa usafi, usahihi na usanifu wa lugha hii umedumishwa sawa na hali inavyojitokeza tunaporejelea lugha nyingine ulimwenguni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kijeruman, Kilatini na kadhalika. Lengo hili litatimizwa ikiwa ufundishaji wa Kiswahili utazingatia matumizi ya sarufi sahihi na mbinu bora za kufundishia katika viwango vyote vya elimu. Jambo ambalo Ligami (2002) analisisitiza, kando na kulaumu njia zilizopo za ufundishaji zisizoridhisha. Mbinu kongwe za ufunzaji wa lugha pia zinawenza kuwa ni sababu nyingine inayopelekeza kuzorota kwa kiwango cha Kiswahili. Ligami (khj) akimnukuu Adedeji (1982) katika mapendekezo ya ufunzaji wa Kiyoruba nchini Nigeria, anaeleza kuwa ufunzaji bora wa lugha ni lazima uanzie kwenye viwango vya chini vya shule, ambavyo ni shule za malezi (chekechea).

MacArthur (1983) anadai kuwa ufundishaji ni sanaa, na hivyo, ufanisi wake hutegemea ufanisi wa kibinaksi wa mwalimu. Mwalimu mzuri anaweza kubadili mwanafunzi asiyejimudu na kumpa uhai. Vile vile, anadai, mazingira huathiri kazi ya mwalimu anapotekeleza majukumu yake darasani. Ni kutokana na hali hii ya mambo ambapo mwandishi wa makala haya anadai kuwa mazingira ya Chuo Kikuu cha Moi yanaathiri matumizi ya Kiswahili. Kiswahili kinachozungumzwa chuoni ni kile kisichojali sarufi ya Kiswahili Sanifu. Kwa hivyo, mwanafunzi wa Kiswahili hapa chuoni anapigwa vita na Kiswahili hiki kisicho sahihi. Hivyo, anatakikana ajitahidi kupambana na athari hizi. Katika ufundishaji wa lugha, MacArthur (1983: 96-102) ametoa mbinu na mikabala mbalimbali ya kutumia:

- i) Mbinu ya Sarufi-Tafsiri.
- ii) Mbinu ya moja kwa moja.

- iii) Mbinu za kimuundo na mikabala mbalimbali.
- iv) Mkabala wa hali.
- v) Mkabala wa mawasiliano.
 - a) Mbinu hii ya sarufi-tafsiri ndiyo kongwe zaidi kama anavyodai MacArthur na inajumuisha matumizi ya vitabu sahihi vyenye vielelezo na sheria sahihi, vipo vya kiada vyenye maelekezo ya kusoma na mazoezi.
 - b) Mbinu ya moja kwa moja iliasisiwa na wanaisimu Francois, Gouin, Welhem Vietor, Otto Jespersen, na Maximilan Berlitz. Hawa walipendekeza, kufundisha lugha kwa mujibu wa lugha hai iliyopo. Lugha hai ni lugha inayotumika kila siku na wanafunzi ajifunze lugha hii. Jambo hili litafanya wanafunzi kupata ule uhai wa lugha. Watumie lugha bila matumizi ya sarufi fafanuzi.

Mawazo haya ya pili, kwa maoni yangu hayana mashiko kwani wanafunzi wanapojojifunza lugha kwa mujibu wa matumizi yaliyopo katika jamii, huharibu sarufi na usahihi wa lugha lengwa. Mfano mzuri uko hapa nchini Kenya ambapo matumizi ya Sheng yamekuwa na athari hasi kwa Kiswahili. Mbinu hii inasisitiza kujifunza lugha kwa kutumia maongezi na kusikiliza. Aidha, kutumia vifaa vifaavyo ambavyo vitawawezeha wanafunzi kujifunza lugha. Mbinu ya moja kwa moja ilipendekeza ufundishaji wa sarufi, msamiati, na vipengele vya fonetiki ya lugha.

Mkabala wa hali uliotokana na nadharia ya maana ya mwanaisimu Mwingereza John Rupert Firth aliyesisitiza umuhimu wa muktadha na hali. Alipendekeza matumizi ya msamiati na ruwaza yenye maana katika yale yanayofuatwa na watu katika maisha yao. Hivyo vifaa vya kusikiliza, michezo, drama, nyimbo, ushairi simulizi na mazoezi yanasisitizwa kufundishia lugha. Firth akasema kuwa mtu hujifunza lugha vyema kwa kufanya mazoezi, na mazoezi haya yawe na umuhimu katika maisha ya wanafunzi nje ya shule.

Mkabala wa mawasiliano unatokana na maoni ya mwanasosholojia Dell Hymes (MacArthur, 1983) kwamba lazima tutalii umilisi wa kuwasiliana kwa dhati kama vile tunavyotalii umilisi wa kiisimu. Kutokana na maoni haya, wananaadharia J. L. M. Trim, David Wilkins na Henry Widdowson waliuita 'uamilifu-kidhana' (notional-functionalism). Kwa hiyo, 'dhana' ni jinsi tunavyousawiri ulimwengu na 'uamilifu' ni jinsi tunavyotaka kuweka, kueleza, na kubadilisha chochote katika hali tunazojikuta tumo. Hii inaashiria matumizi ya lugha katika hali fulani na muktadha. Kwa hiyo, wanafunzi wanatarajiwa kufahamu matumizi ya msamiati wa lugha katika miktadha mbalimbali ili kuwasiliana ipasavyo.

Mbinu na mikabala hii inatumika katika viwango vyote vya kujifunza lugha kutoka shule za msingi, upili na vyuo vikuu. Hata hivyo, mitalaa huzingatia kuzamia taaluma ya Kiswahili baada ya wanafunzi kujifunza sheria za kimsingi za

Kiswahili kama vile umoja na wingi, uambishaji, urejeshi, uonyeshaji, umilikishi, njeo, kauli mbalimbali na miundo tofautitofauti ya sentensi. Swali ni je, wanafunzi wetu wanapofika chuoni wamefanikiwa kujifunza haya?

Uchanganuzi wa Data

Mwandishi wa makala haya alitumia kazi za wanafunzi za mtihani kutoka mwaka wa kwanza hadi wa nne [jumla ya wanafunzi mia nane na sitini na nane (868)] kudadisi na kutathmini umilisi wao wa sheria za msingi za sarufi ya Kiswahili tulizozitaja hapo juu. Kutoka kundi hili, mtafiti alichagua vijitabu vyatay majibu thelathini (30) katika kila mwaka, na kuibuka na vijitabu mia moja na ishirini (120) vyatay wanafunzi mia moja na ishirini (120). Uteuzi huu ulifanywa bila kuzingatia mfumo maalumu. Katika kazi hizi, mtafiti alichanganua matatizo ya sarufi katika kazi zao alizoziteua. Matatizo ya sarufi yaliyochunguzwa yalizingatia uambishaji, umilikishi, urejeshi, uashiriaji na maendelezo kutokana na matamshi. Maendelezo yalidhihirisha matamshi yasiyo sahihi.

Uambishaji

Uambishaji ni msingi mmojawapo wa lugha za Kibantu. Ujuzi wa viambishi vyatay aina mbalimbali ni lazima katika kuielewa lugha yoyote ya Kibantu (Kapinga, 1983; Nkwera 1978). Kaffka (1985) anasema kuwa Kiswahili ni lugha ambishi, na kwa hiyo, uambishaji sahihi huleta upatanisho wa kisarufi katika lugha za Kibantu, Kiswahili kikiwemo.

Kapinga (kama hapo juu) anaeleza kwamba kiambishi ni mofimu inayoambatishwa kwenye mzizi au shina la neno ili kulitambulisha neno lenyewe. Viambishi vyatay ngeli huambatishwa kwenye viini au mashina ya maneno ya fungu moja yakiwa katika upatanisho wa kisarufi. Maneno yanayoingia katika upatanisho wa kisarufi ni majina/nomino, vivumishi, viwakilishi na vitenzi. Jina/Nomino ndiyo inayoambatisha kiambishi chake kwenye maneno mengine katika sentensi iwe katika hali ya umoja au wingi. Hivyo tunasema, KN ndiyo hutawala viambishi katika sentensi. Munyua (1992) anaiita dhana hii ya uambishaji kama uwakilishaji. Anaeleza kuwa ni kanuni ya kisarufi inayoletea KN iliyokwisha kutajwa katika matamshi ya awali, kwa mfano sentensi za awali, kishazi au vishazi vyatay awali, kuwakilishwa kwa 'elementi wakilishi', yaani, maumbo wakilishi au viwakilishi. Viwakilishi hivi vyatay KN ndivyo huitwa viambishi na lazima vitumike kwa mujibu wa ngeli ya KN ili sentensi iwe sahihi kisarufi. Viambishi sahihi vyatay KN katika ngeli yake lazima vitumike. Iwapo havitatumika hivyo, sentensi hiyo haikubaliki kisarufi:

1. a) Mwalimu amenunua gari jipya (umoja).
- b) Walimu wamenunua magari mapya (wingi).

Katika mfano huu (1a & b), **Mwalimu** ndiyo nomino na kiambishi chake ni **a-** katika kitenzi "-nunua" na **gari** ni nomino na kiambishi chake ni **ji-** katika kivumishi "-pya".

Wanafunzi wengi tuliovatitnia hawana umilisi wa sheria hii katika Kiswahili. Miogoni mwa wanafunzi mia moja na ishirini waliosampulishwa, asilimia tisini na tano (95%) hawana umilisi wa uambishaji. Tudurusu baadhi ya mifano hii:

2. *Hadithi **waweza** kuwa hurafa au hekaya.
3. *Dini pia **ilimetumika** kumkandamiza mwanamke katika jamii.
4. *Utamaduni **imeleta** ukandamizaji wa mwanamke.
5. *Wanaume wanaishia ulevini na **kuvitumia** pesa zao katika ulevi.

Hii ni baadhi ya mifano ya makosa mengi ya uambishaji yaliyopatikana katika kazi za wanafunzi. Makosa haya yalitamalaki kuliko makosa yoyote mengine. Uambishaji ni jambo la msingi katika Kiswahili na huanza kufundishwa katika mtalaa wa shule za msingi (darasa la kwanza hadi la nane) na kuendelezwa katika shule za upili (kidato cha kwanza hadi cha nne) kabla ya mwanafunzi kuijunga na Chuo Kikuu (miaka minne). Hili ni jambo la kushangaza na kusikitisha sana kwamba wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu hawana umilisi wa sheria hii ya kimsingi katika sarufi ya Kiswahili waliyoisoma kwa miaka kumi na miwili (12) kabla ya kuijunga na Chuo Kikuu.

Umilikishi

Umlilikishi ni hali ya kuonyesha umiliki wa kitu (Nomino) katika sentensi. Habwe na Karanja (2007) wanaeleza kuwa katika Kiswahili kuna viwakilishi milikishi ambavyo huundwa kwa mofimu za umilikishi -angu, -etu, -ako, -enu, -ake, -ao zikitumiwa na viambishi vya upatanisho wa ngeli. Kapinga (1983) anaeleza kuwa maneno ya vimilikishi huweza katika aina ya maneno ya vivumishi yakinumia pamoja na majina (mtazamo wa Kapinga ni kwa mujibu wa uamilifu wa vimilikishi katika sentensi - katika makala haya ninaviangalia kama vimilikishi). Wanafunzi asilimia themanini na tano (85%) walionyesha ukosefu wa kufahamu matumizi sahihi ya vimilikishi. Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya makosa hayo:

6. *Mtambaji hadithi anaweza kuuliza maswali, kutoa mjadala na pia katika kuimba na **hadhira wake**.
 7. *Mwandishi **anaweza maliza** kwa kuimba anapomaliza hadithi **wake**.
 8. *Anaweza kuvalaa piku katika kichwa **yake**.
-

Mifano hii inadhihirisha makosa ya vimilikishi visivyo sahihi katika sentensi. Vimilikishi pia huambishwa mofimu kwa mujibu wa ngeli ya KN. Wanafuzi wengi wanatumia vimilikishi bila kujali ngeli ya KN. Ifahamike kuwa katika Kiswahili, KN ndiyo hutawala viambishi katika sentensi, yaani ndiyo huongoza viambishi gani vya kutumia kuleta usahihi wa sentensi.

Urejeleaji

Makoti (2013:17) anaeleza, "Urejeleaji ni ile hali ya maumbo fulani ya lugha kutumiwa kurejelea faridi fulani za kiisimu ambazo ama hutokea mwanzoni mwa matini au baadaye. Faridi hizo husimamiwa na virejelea vinavyowakilisha maumbo hayo. Virejelea hivi pia huitwa vionyeshi. Vionyeshi hivi katika Kiswahili hutawaliwa na KN". Habwe na Karanja (2003) wanaeleza kuwa katika Kiswahili, vionyeshi vinaweza kufanya kazi ya vivumishi, viwakilishi na vibainisho. Vionyeshi hivi, katika Kiswahili, huambishwa mofimu za ngeli ya nomino ili kurejelea uhusiano wa ujirani wa watusika katika sentensi. Mfano wa vionyeshi ni *huyu, hiki, zile, lile* na kadhalika. Vionyeshi visipozingatia ngeli ya KN, sentensi hiyo haikubaliki kisarufi. Ifuatayo ni mifano ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi:

9. *Mshororo wa mwisho umerudiwa rudiwa ambaye ni, 'Ewe Mola wa ...'
10. ***Mhusika huu** ni mhusika ambaye ana sifa za kibinadamu.
11. *Pia hadithi **huo** wa Pwaguzi kuna monolojia.
12. *Mtambaji anaweza kuvaav mavazi ya sungura kulingana na hadithi anachosimulia.
13. *Vina vya mishororo **yale** mengine ni ...

Mifano hii ni baadhi tu ya makosa yanayofanywa na wanafunzi Chuoni. Asilimia themanini na tano (85%) ya wanafunzi watafitiwa walifanya makosa haya.

Matamshi/Maendelezo

Matamshi ni jinsi ya kutamka maneno ya lugha fulani. Matamshi haya lazima yawe kama yanavyotamkwa na wazawa wa lugha hiyo. Matamshi huenda sambamba na maendelezo ya maneno. Tunapotamka maneno visivyo, maendelezo nayo hupotoka. Tuchunguze makosa ya maendelezo ambayo yamerandana na matamshi yaliyofanywa na wanafunzi watafitiwa:

14. *Wakene alipogundua kwamba ombi la kumridhi (kumrithi) Natala kama mke wa pili **umekonga** (umegonga) mwamba, alikata tamaa.

15. *Mchezo inapoanza, tunamwona Kinaya, bwanake Mwavita **akikonga** (akigonga) mlango saa tisa asubuhi.
16. *Mwanamke **angeruhusiwa** (hangeruhusiwa) kupiga kura. (sentensi hii inatakikana iwe kanushi lakini haikuwa hivyo kwa sababu ya matamshi na maendelezo).
17. *Nyalwe anaondoka na Bokono **anapaki** (anabaki) peke yake.
18. ***Tamtilia** ya Amezidi inadhihirisha... (kosa hili hujitokeza daima dawamu, hata katika kiwango cha Uzamili).

Makosa haya yanatokana na kutofahamu vyema fonolojia ya Kiswahili na pia yanaendana na athari za lugha ya kwanza. Makosa haya yalifanywa na asilimia arobani (40%) ya wanafunzi watafitiwa. (Mtafiti hakuzingatia kabilia za watafitiwa, wala hakujua majina yao. Vijitabu vya majibu vya wanafunzi huwekwa nambari ya usajili tu).

Uakifishaji

Wanafunzi asilimia tisini (90%) hawafahamu uakifishaji sahihi. Walidhihirisha kutofahamu matumizi ya herufi kubwa na ndogo, matumizi ya koma, alama za kunukuu, ritifaa na upangaji aya:

- a) watu wasio wa rangi moja kama vile kule marekani wana **Lahaja** ya Kiingereza. **wamarikani** weusi wana lahaja yao na wale weupe wana yao.
- b) mazingira tofauti linabuni lahaja tofauti. Kama vile watu waliotoka pwani wana lahaja tofauti tofauti. Matukio ya kihistoria kama vile vita. Ambapo watu jamii huangamia. Baada ya vita jamii mpya huundwa. wanajamii hawa hubuni Lugha nyininge ambayo ni lahaja ya Lugha asili yao.
- c) Uwezo wa kutumia nomino katika lugha ukielezea jinsia. Ni jinsi ya maneno ya mwanamke kutofautiana na maneno yanayosemwa na wanaume utapata kuwa mwanamke anweza kusema au kuongea kwa maringo ilhali mwanaume hawezi kuongea kama ako na maringo ya kutingisha kichwa na kutumia vidole akiashiria hewani kama vile mwanamke anafanya. Kimbo cha mwanamke hutofautiana na kile mwanamume. Ata kataika mavazi utapata kuwa mwanaume hawezi akavalia kama mwanamke kwa mfano mwamume kuavalia rinda au viatu vya wanawake na akifanya hivyo basi hawezi kuwa sawa Vile vile mwanamke hawezi kukaa au kuvalia kama mwanaume na akifanya hivyo basi anaweza kuwa shoga. Kulingana na tabia yake ambayo ni ya kiume ilhali yeye ni mke (*Mifano hii a), b), c) ilinukuliwa kama ilivyo katika kazi za wanafunzi. Si makosa ya mtafiti*).

Tukichunguza mifano hii mitatu a), b) na c), makosa ya vipengele mbalimbali vya uakifishaji yanadhihirika. Hii ni baadhi tu ya mifano kutoka kazi hizo za wanafunzi zilizoteuliwa kama sampuli.

Marejeleo/Vitabu vya Kiswahili Maktabani Chuoni

Tuligundua yafuatayo:

- i) Maktabani katika eneo la maazimo ya muda mfupi, hakukuwa na kitabu hata kimoja cha Kiswahili.
- ii) Katika sehemu ya kusomea, kulikuwa na vitabu tofauti tofauti vya fasihi na lugha, nakala kumi na nane [fasihi nakala kumi na mbili (12) na lugha nakala sita (6)]
- iii) Sehemu na *National Collections*, kulikuwa na tasnifu za Kiswahili saba (7) na vitabu vya fasihi na lugha sita (6).

Kwa hivyo hivi ndivyo vitabu vya Kiswahili maktabani Margaret Thatcher, chuoni.

Walimu katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Idara hii ina wahadhiri wa Kiswahili kumi na wawili (12) akiwemo Profesa mmoja. Kuna wahadhiri waliofuzu uzamifu watano (5), uzamili wanenye (4) na wanafunzi wandamizi wawili (2). Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wa somo la Kiswahili, walimu hawa hawatoshelezi mahitaji ya idara hii. Mfano, wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliosoma somo la Kiswahili EDK 100: *Introduction to Kiswahili Language and Linguistics* walikuwa mia tatu na hamsini na nne (354) mwaka wa 2013/2014; wanafunzi wa mwaka wa pili waliosoma BKS 211: Oral Literature in Kiswahili walikuwa mia nne na thelathini na tano (435) mwaka wa 2013/2014. Tunapoangalia idadi hii kubwa ya wanafunzi, ikilinganishwa na idadi ndogo ya walimu idarani, ingekuwa bora walimu zaidi waajiriwe kwa lengo la kupunguza mzigo kwa walimu waliopo ili waweze kutayarisha masomo yao vyema na kuitia kazi za wanafunzi kwa uangalifu zaidi.

Hitimisho na Mapendekezo

Umilisi wa lugha ni muhimu katika kuendeleza lugha sahihi katika jamii (zikiwemo shule za viwango vyote). Kwa vile wanafunzi wengi wanaosoma Kiswahili ni wale wanaotarajia kuwa walimu, lazima waimudu lugha na sarufi yake. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, kuna changamoto nyingi katika ufundishaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi. Kwanza, wanafunzi wengi wanakosa ufahamu wa sheria za kimsingi za sarufi ya Kiswahili. Jambo hili ni tatizo kubwa na sugu kwa sababu mtalaa wa Chuo Kikuu haushughuliki na viwango vya chini katika Kiswahili. Kwa hiyo, wanafunzi hawa huendeleza makosa yao kutoka shule za upili.

Ukosefu wa vitabu vya marejeleo na kusoma kwa jumla maktabani, unachangia pakubwa kwa kuendelezwa kwa makosa haya ya kisarufi na wanfunzi. Vitabu vingekuwewo, wanafunzi wangejisomea na kujifunza zaidi na kujirekebisha. Tatizo la idadi kubwa ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni na idadi ndogo ya wahadiri, ni tatizo kubwa. Mfano, mwaka wa kiakademia (2013/2014) mtafiti alikuwa na darasa la wanafunzi wa mwaka wa nne mia tatu na thalathini (330) katika somo la KIS 411: Modern Kiswahili Poetry na wa mwaka wa tatu mia tatu na sabini na tano (375) katika somo la BKS 320: Literary Devices and Criticism. Ifahamike kwamba ni vigumu sana kuwa na uzingatifu kwa kila mwanafunzi katika idadi kubwa kama hii. Hakuna mtagusano wa moja kwa moja wa mawasilisho ya wanafunzi ili kuwasikiliza na kuwarekebisha wafanyapo makosa. Mazingira chuoni ni yale ya matumizi ya Sheng na Kiswahili kisicho sahihi. Mambo haya yanachangia pakubwa kwa wanafunzi kutokuwa na umilisi wa kanuni za kimsingi za sarufi ya Kiswahili. Lugha anayosikia mtu na kuiongea ndiyo aandikayo katika matumizi yake ya kila siku. Kukabiliana na changamoto hizi, hapa ninatoa mapendekezo:

- i) Maktaba inunue vitabu zaidi vya Kiswahili ili kufikia kiwango cha maktaba ya Chuo Kikuu, vya lugha/sarufi na fasihi.
- ii) Wanafunzi wasome zaidi vitabu vinavyozamia sarufi ya Kiswahili. Wasome pia vya fasihi na wajikite zaidi katika matumizi ya lugha.
- iii) Wanafunzi wasomao Kiswahili Chuoni, wajikinge na athari ya Sheng na matumizi yoyote ya Kiswahili yasiyo sahihi. Hili watalifikia tu, iwapo watasoma sarufi ya Kiswahili kwa dhati ili kuyapambanua makosa hayo.
- iv) Vitabu vya kimsingi vya sarufi ya Kiswahili vipatikane maktabani.
- v) Vikao vya ushauri na mijadala kati ya walimu na wanafunzi vianzishwe ama visisitizwe Chuoni ili washauriane juu ya lugha sahihi na kupiga msasa Kiswahili chao.
- vi) Mashindano ya mazungumzo hadharani na ya uandishi Chuoni yaanzishwe na zawadi kutolewa ili kuwahamasisha wanafunzi juu ya matumizi sahihi ya Kiswahili.

Marejeleo

- Barongo, S. (1996). "Mshikamano katika Insha za Wanafunzi wa Kidato cha Nne katika Wilaya ya Gusii". Tasnifu ya Uzamili (MPhil.), Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret (Haijachapishwa).
- Brown, K. na Jim, M. (1991). *Syntax: A Linguistic Introduction to Sentence Structure*. London: HaperCollins Publishers.
- Chimera, R. (2000). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Eshiwani, G. (1993). *Education in Kenya Since Independence*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2003). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hesplemath, M. na Andrea, D. S. (2010). *Understanding Morphology*. 2nd edition, London: Hodder Education.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Ligami, P. (2002). "Ujuzi na Utendaji katika Kiswahili: Umuhimu wa Utafiti" katika Simala (mhr): *Utafiti wa Kiswahili*, Eldoret: Moi University Press kur 136-140.
- Makoti, V. S. (2013). "Mshikamano wa Kisarufi katika Kiswahili", Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. Tasnifu ya Uzamifu (PhD) (Haijachapishwa).
- Mbaabu, I. (1988). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Ltd.
- McArthur, T. (1993). *A Foundation Course for Language Teachers*, Cambridge: Cambridge University Press.
- Mgullu, R. (1999). Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili, Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Mohamed, A. M. (2001). *Modern Kiswahili Grammar*, Nairobi: East Africa Educational Publishers.

- Munyua, J. G. (1992). "Uwakilishaji wa Nomino katika Kiswahili" Chuo Kikuu cha Moi Eldoret, Tasnifu ya Uzamili (MPhil.) (Haijachapishwa).
- Obuchi, S. M. na Mukhwana, A. (2015). Muundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Odeo, I. (2002). "The Future of Kiswahili Classroom Research" katika Simala (mhr) *Utafiti wa Kiswahili*, Eldoret: Moi University Press kur 128-135.
- Ogechi, N. (2009). "The Teaching of Kiswahili in Kenyan Universities with Emphasis on Histography" katika *IFRA-Le Chashirs, No. 40*, kur 151-165.
- Ogechi, N. (2004). "Athari ya Mabadiliko ya Mitalaa katika Uchapishaji wa Kiswahili Nchini Kenya" katika *Swahili Forum XII*, kur 92-104.
- Okech, J. G. na Asiachi, A. J. (1986). *Curriculum Development for Primary Schools in Kenya*. Nairobi: Kenyatta University.
- Ondiek, P. E. (1986). Curriculum Development: Alternatives in Educational Theory and Practice. Kisumu: Lake Publishers and Enterprises.
- Tellerman, M. (2011). *Understanding Syntax*. London: Hodder Education.
- Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers .